# JARIDA LA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

UMITASHUMTA UMISSETA

**Toleo la Mtandaoni: 13** | 16 Agosti, 2022 - TABORA | www.michezo.go.tz


## VINARA KUKUTANA FAINALI UMISSETA 2022



Wizara_SanaaTz

# VINARA KUKUTANA FAINALI UMISSETA 2022

16 Agosti, 2022




# Robo Fainali Mpira wa Kikapu UMISSETA 2022

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) kitaifa yanayoendelea mkoani Tabora, mpira wa kikapu umetinga hatua ya robo fainali.

Katika Mchezo uliowakutanisha Dar es Salaam na Mjini Magharibi, (Wavulana) Dar es Salaam imeichapa Mjini Magharibi vikapi 99 kwa 44, ambapo Arusha wamewaadhibu Tanga Vikapu 88 kwa 80.

Kwa upande wa Wasichana, mchezo uliowakutanisha wenyeji Tabora na Rukwa, Tabora imewagalagaza Rukwa vikapu 43 kwa 10.

Mechi nyingine iliyowakutanisha Mwanza na Ruvuma (Wasichana), Mwanza imeichapa Ruvuma vikapu 46 kwa 39.

Mechi za nusu fainali zinatarajiwa kuchezwa Agosti 17, 2022 Viwanja wa Sekondari ya Wavulana Tabora.



# Mchezo wa Mpira wa Mikono wakamilisha hatua ya Robo Fainali

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mchezo wa Mpira wa Mikono (HandBall) katika Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) kitaifa yanayoendelea mkoani Tabora, umeingia hatua ya Robo Fainali.

Katika michezo iliyochezwa Agosti 16, 2022, viwanja vya Sekondari ya Wasichana Tabora, kwa upande wa Wavulana Mkoa wa Mjini Magharibi wameiadhibu Mbeya magoli 37 kwa 29.

Katika mchezo mwingine, Arusha wameichapa Tanga magoli 33 dhidi ya 31, huku Songwe akiiadhibu Dar es Salaam magoli 18 dhidi ya 16 nao Mkoa wa Morogoro umeufunga Mkoa wa Mara magoli 18 dhidi ya 12.

Nusu fainali ya mchezo huo, itawakutanisha Mjini Magharibi dhidi ya Songwe na Morogoro dhidi ya Arusha.

Kwa upande wa Wasichana, Shinyanga imeibamiza Dodoma magoli 18 dhidi ya 17, huku Songwe wakiikalisha Tabora Morogoro magoli 26 kwa 08 nao Mkoa wa Morogoro umeiadhibu Katavi magoli 25 kwa 09.

Michezo ya nusu fainali itachezwa Agosti 17, 2022 viwanja vya Sekondari ya Wasichana Tabora, kwa Morogoro dhidi ya Songwe na Shinyanga dhidi ya Geita.



# Dodoma na Tanga Mabingwa Kurusha Mikuki UMISSETA 2022

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mkoa wa Dodoma umeibuka Bingwa katika mchezo wa Kurusha Mikuki upande wa Wavulana kupitia mwanafunzi Elisha Reiya aliyerusha kwa mita 56 kwa sentimita 95, hukub Tanga ikiibuka Bingwa upande wa Wasichana kupitia Marietha Charles aliyerusha umbali wa mita 39 kwa sentimita 25.

Mabingwa hao wamepatikana Agosti 16, 2022 katika Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) yanayoendelea mkoani Tabora.

Mkoa wa Mwanza umeibuka mshindi wa pili kwa upande wa Wavulana kupitia Yohana Nicolous aliyerusha mita 51 kwa sentimita 72, huku nafasi ya tatu ikienda Dar es Salaam kupitia Risa Sereny umbali wa mita 49 kwa sentimita 65.

Kwa upande wa Wasichana, nafasi ya pili imekwenda Mkoa wa Pwani kupitia mwanafunzi Eliza Keraryo aliyerusha mita 35 kwa sentimita 10, huku nafasi ya tatu ikienda Manyara kupitia Maria Gemariri mita 34 kwa sentimita 95.

Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) inatarajiwa kuhitimishwa Agosti 19, 2022 Mkoani Tabora.



# Wanafunzi Wachuana Vikali Netiboli UMISSETA 2022

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mchezo wa Netiboli umetinga Robo Fainali katika Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) yanayoendelea Mkoani Tabora.

Michezo iliyochezwa Agosti 16, 2022 Mwanza imeiadhibu Tabora kwa magoli 44 dhidi ya 35 na kuipa Mwanza tiketi ya kutangulia nusu Fainali.

Katika mchezo mwingine Mkoa wa Songwe umeigalagaza Mkoa wa Dar es Salaam magoli 92 Kwa 24, huku Geita ikiiadhibu Dodoma magoli 77 kwa 25, nao Mkoa wa Iringa umeuchapa mkoa wa Mbeya magoli 50 Kwa 27.

Mechi za Nusu fainali zitawakutanisha Mkoa wa Mwanza dhidi ya Geita, pamoja na Songwe dhidi ya Iringa, Agosti 17, 2022 viwanja vya Sekondari ya Wasichana Tabora.




# Sanaa za Jukwani, Mikoa Yachuana Katika Ngoma za Asili UMISSETA

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Mashindano ya Sanaa za michezo katika kipengele cha ngoma za asili kwa Vijana wa Shule za Sekondari nchini Tanzania yameingia hatua ya fainali Agusti 16, 2022 katika ukumbi wa chuo cha ualimu Tabora Agust 16, 2022.

Sanaa na Michezo ni sehemu ya michezo iliyojumuishwa katika michezo ya UMISSETA 2022 ambapo jumla ya mikoa tisa imehusika katika nusu fainali ili kumtafuta Bingwa ambaye Mkoani wake utaibuka kidedea.

Mikoa Tisa ambayo imeshindana katika hatua ya fainali ni Dodoma, Shinyanga, Mwanza, Njombe, Lindi, Mtwara, Pwani, Kagera na Arusha ambayo vikundi vyake vilionyesha uwezo wa kucheza ngoma za asili za mikoa mbalimbali ya Tanzania.
Matokea ya Bingwa wa Mkoa ulioshinda atatangazwa Agusti 17, 2022 baada ya majaji wa mashindano kukamilisha kazi yao ya uchataji wa matokeo.

Fainali hiyo imefuatiwa na mchuano mkali wa awali uliohusisha Mikoa 27 ambayo ilionyesha umahiri katika sanaa za michezo kipengele cha kuimba kwaya.

Sanaa za michezo zimeonyesha kuvuta watazamaji wengi katika mashindano ya UMISSETA 2022 kutokana na vipaji vinavyoonyeshwa na vijana wa shule za sekondari kutoka mikoa mbalimbali nchini katika fani za ngoma, kwaya na muziki wa kizazi kipya (Bongo Flavour).




# Sanaa za Jukwaani Zaingia Hatua ya Fainali UMISSETA

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Mikoa Tisa iliyoingia hatua ya fainali katika mashidano ya Sanaa za Jukwani kipengele cha kwaya imechuana Agosti 16, 2022 katika hatua ya fainali ili kumpata mshindi.

Fainali hiyo imefanyika katika ukumbi wa Chuo cha Ualimu Tabora, na kuikutanisha mikoa ya Tabora, njombe, Kagera, Iringa, Rukwa, Mbeya, Kigoma, Mtwara na Tanga.

Fainali hiyo imefuatiwa na mchuano mkali wa awali uliohusisha mikoa 27 ambayo ilionyesha umahiri katika kipengele cha kuimba kwaya.

Matokeo ya washindi wa fainali yanatarajiwa kutangwazwa August 17, 2022 kwenye ukumbi wa Tabora TTC ambapo pamoja na kwaya lakini pia atajulikana bingwa wa Ngoma za asili.

Mwalimu Erasto Lihawa ambaye ni mkufunzi wa wa Sanaa za Michezo kutoka Mkoa wa Njombe ameeleza mashindano hayo kuwa sehemu ya masomo kwa wanafunzi ambayo yanalenga kuwaongezea fursa katika maisha yao.

"Sanaa ni elimu, ajira na furaha hivyo vijana wetu kutoka mikoa mbalimbali wanaoshiriki mashindano haya wamepata vitu vya ziada ikiwepo kujiandalia mazingira ya kujiajiri kupitia uimbaji" amesema Mwalimu Erasto.

Naye Mwalim Mbalu Mathias kutoka kikundi cha kwanya cha Mkoa wa Tabora ameishauri Serikali kuona namna ya kuwaendeleza vijana wanaoonekana na vipaji mbalimbali wakati wa UMISSETA.

Amesema kupitia vipaji vya wanafunzi vinavyoonekana kwenye Sanaa za michezo, zipo taasisi mbalimbali nchini ambazo kwa kushirikiana na Serikali zinaweza kuwaendeleza wanafunzi hao ili dhana ya michezo ni ajira ionekane kwa vitendo.

"Vipaji vya vijana hawa havitakiwi kuachwa hivihivi, vinapaswa kufanyiwa kazi ili hata wale ambao hawajashiriki wahamasike kushiriki kwa kuwaona wenzao wananufaika kwa namna flani kupitia vipaji vyao" amesema Mwalimu Mbalu.

# UMITASHUMTA | UMISSETA
# 2022

# #SensaBika

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo